

## LEARNING BY EAR 2009

### Economics – 2nd episode

#### SUCCEEDING IN THE BUSINESS WORLD

**Series:** “THE STORY OF TWO YOUNG PEOPLE, WHOSE SUCCESS STEMS FROM THEIR POCKET MONEY”

**Author:** Frédéric GAKPARA

**Editors:** Yann Durand and Sandrine Blanchard

**Translator:** Anne Thomas

**Kisuaheli :** Eric Ponda

#### SECOND EPISODE: “Holidays well-spent”

**Characters :** John (*16-year-old boy, twin.*)

Jane (*John's twin sister.*)

1<sup>st</sup> customer (*Young man, 30ish, spectator.*)

2<sup>nd</sup> customer (*Young man, 20ish, gambler resting.*)

3<sup>rd</sup> customer (*Woman, 40ish, waiting for a taxi.*)

4<sup>th</sup> customer (*Man, 50ish, manager of bar-restaurant.*)

Narrator

**Learning by Ear Soundtrack**

[Intro](#)

**NARRATOR:** Ni wakati mwengine tunapoungana tena kukuletea makala haya ya Learning by Ear “Noa bongo jenga Maisha yako, wakati huu tukinoa bongo na masuala ya Uchumi. Ni hadithi kuhusu ufanisi wa vijana wawili wanaojikakamua kutimiza ndoto yao ya kuwa wanauchumi mashuhuri, kwa kubania pesa zao za matumizi .Katika makala haya, John na Jane ambao ni mapacha, wanajitosa katika ulimwengu wa biashara ya kuuza njugu karanga. John anaanza bishara hiyo kuwauzia wateja walioko mapumzikoni katika ufuo wa Bahari ilhali Jane anaeleka katika sehemu za burudani hususan kwenye Mabaa, mikahawani na barabarani.

**Scene 1, AT THE BEACH**

JOHN, 1<sup>st</sup> CUSTOMER, 2<sup>nd</sup> CUSTOMER

**ATMO:** *We can hear the sound of the waves breaking. In the distance, people are playing football. Spectators are spurring them on. Others are swimming (shouts and laughter).*

1. **John:** (*Shouting*)  
...Njugu! Njugu! Njugu tamu.. za chumvi..  
Njugu... Njugu...!

2. **1<sup>st</sup> customer:** Wewe Mvulana, hebu lete hizo Njugu karanga.

3. **John:** ...Njugu..! Njugu..! Njugu za chumvi Njugu....!

....

4. **1<sup>st</sup> customer:** Wewe ni kiziwi au nini.? Nakuita hapa na wewe unaendelea kuimba Njugu..! Njugu...! huna heshima ?
5. **John:** Samahani usikasirike.. Sikusikia Mzee!
6. **1st customer:** Sawa?
7. **John:** Hata anapokuwa na mteja mzee, mfanyi biashara lazima ataendelea kutangaza biashara yake kutafuta mteja mwengine.! Wimbo wa kuitangaza biashara utafika kikomo atakapo hakikisha ameuza kila kitu.
8. **1<sup>st</sup> customer:** Wewe ni kijana mwerevu sana.! Na nafurahishwa na ujasiri wako. Ni pesa ngapi?
9. **John:** Faranga 20 tu Mzee!
10. **1<sup>st</sup> customer:** Hizi njugu zako ni tamu?
11. **John:** Tena sana .... Utazipenda!
12. **1<sup>st</sup> customer:** Sawa...! Na kweli zina chumvi! Nipe pakiti tatu.
13. **John:** Hizi hapa Mzeel... Na hii chenji yako Mzeel.

14. **1<sup>st</sup> customer:** Ahhh weka tu ! hiyo ni bakshishi yako..
15. **John:** Asante sana Mzee!..... Haya Njugu...!  
Njugu,,! Njugu tamu za Chumvi..!
16. **2<sup>nd</sup> customer:** Wewe mvulana nipe Njugu... Ni tamu?
17. **John:** Ni tamu sana mzee!. Zina chumvi, ....  
Utazifurahia!
18. **2<sup>nd</sup> customer:** (*After munching on some groundnuts.*)  
Uuuum! Ni tamu sana ! Hebu nipe pakiti  
nne.... Unaziuzaje?
19. **John:** Pakiti nne ni faranga 100.. Hizi hapa mzee!...  
Asante sana!  
(*Shouting*)  
...Tamu Njugu... Njugu Tamu... Haya Njugu..  
.....Njugu!
20. **2<sup>nd</sup> customer:** Wewe mvulana, ngoja kidogo! Nipe pakiti  
nyingine mbili!
21. **John:** Bila shaka, Haya ndio hizi hapa ! (*Shouting*)  
Njugu... Njugu za Chumvi njugu! ...Pesa  
Mzee?
22. **2<sup>nd</sup> customer:** Ohhh! ....Pole sana! Pesa hizi hapa kijana!

**23. John:** Asante sana ! Haya njugu... Njugu.. njugu za chumvi Njugu!

**24. ATMO:** *The sound fades gradually.*

**NARRATOR:** Msikilizaji umesikia ujasiri wa John akiuza Njugu zake ufuoni. Hali kadhalika, hatua chache tu barabarani pia biashara inamnogea Dadake Jane ambaye anauza Njugu hizo kwa wateja wa barabarani, Mikahawani na hata kwenye mabaa...!

## SCENE 2, ON THE AVENUE

JANE, 3<sup>rd</sup> CUSTOMER, 4<sup>th</sup> CUSTOMER

**25. ATMO:** *Sound of cars. Horns beeping. Traders selling newspapers shout. Coupé Décalé Music in the bars*

**26. Jane:** (*Shouting*)  
...Njugu... Njugu..... Njugu za Chumvi Njugu!  
Nunua Njugu tamu hapa.... Njugu!

**27. 3<sup>rd</sup> customer:** Wewe msichana, Njugu zako ni kubwa au zile ndogo ndogo tu?

**28. Jane:** Ndio ni kubwa na tamu sana mama!

29. **3<sup>rd</sup> customer:** Hebu nionje kama kweli ni nzuri ... (*After tasting*) Umm! Ni tamu sana, Unauzaje pakiti moja ?
30. **Jane:** Faranga 25 tu Mama!
31. **3<sup>rd</sup> customer:** Nipe za faranga 200 .  
(*Taxi beeps*)  
Fanya haraka ile Texi inanisubiri!
32. **Jane:** Nitakufungia Mama usiwe na wasi wasi...
33. **3<sup>rd</sup> customer:** Hapana wacha kufunga..! Nitaweka kwenye mkoba wangu.  
(*Taxi beeps again*)  
Subiri kidogo!. Sawa pesa zako hizi msichana!.
34. **Jane:** Asante, na uwe na siku njema!
35. **ATMO:** *We hear the sound of the car door shutting and the taxi gets going.*
36. **Jane:** Njugu za Chumvi Njugu.... Njugu Njugu...!
37. **ATMO:** *Coupé Décalé music from a bar-restaurant.*
38. **Jane:** (*Entering the bar-restaurant.*)  
Habari mzee!

- 39. 4<sup>th</sup> customer:** Nzuri nikusaidie na nini?
- 40. Jane:** Nauza Njugu hapa , Ni nzuri sana ukinywa na pombe. Pia ni nzuri kutafuna unaposubiri kuletewa kinywaji Mzee.!
- 41. 4th customer:** Kweli ? Njugu zako zinaonekana nzuri na tamu ? Na unaitwa nani?
- 42. Jane:** Jane.
- 43. 4<sup>th</sup> Customer:** Jane... Wewe unasoma?
- 44. Jane:** Ndio nataraji kuingia daraja la 12.
- 45. 4<sup>th</sup> customer:** Pongezi sana!
- 46. Jane:** Asante sana Mzee..!Ungependa kununua njugu?
- 47. 4<sup>th</sup> customer:** Nakuombea ufanisi Jane.! Endapo wasichana wote wa rika lako hapa mjiini wangekuwa kama wewe, hapana shaka maisha yangebadilika. (*After tasting them.*) Ummm! Ni tamu sana, kwani unazitayarisha vipi Jane? Ni tamu sana!
- 48. Jane:** Asante Mzee, nikuongeze nyingine?

- 49. 4<sup>th</sup> customer:** Niongeze! Na kama unaweza kuziweka kwenye chupa na kuniletea kila wiki ingekuwa bora zaidi. Unaweza kunilitea chupa nne kwa wiki.?
- 50. Jane:** Nitafanya hivyo Mzee! Kiasi unachohitaji Mzee!
- 51. 4<sup>th</sup> customer:** Sawa tumekubalina!
- 52. Jane:** Asante sana na kwaheri mzee!
- 53. 4<sup>th</sup> customer:** Kwaheri Jane na kila la Kheri!
- 54. Jane:** Asante!
- 55. ATMO:** *The sounds of the street and the music fade gradually.*
- NARRATOR:** Hivyo ndivyo mambo yanavyomwendea Jane katika juhudzi zake za kuuza Njugu mjini.

## MUSIC

- NARRATOR:** Ni miezi miwili sasa tangu John na Jane waanzishe bishara yao ya kuuza Njugu mjini. Na katika muda wa wiki zijazo, wawili hawa watarudi shulenii kuendelea na masomo yao, hivyo basi ni lazime wamalize kuuza mali

waliyo nayo kabla ya muda huo kumalizika. Na wanaporejea nyumbani baada ya shughuli za siku, wakiwa chumbani mwao wanajadiliana kwa kina kuhusu suala...

### SCENE 3, IN THEIR ROOM

JOHN AND JANE

**56. ATMO:** *We hear the sound of the door opening and closing. Jane has just arrived, followed by a meowing cat.*

**57. Jane:** John ulitaka kufanya hesabu sasa hivi?

**58. John:** Bora tufanye hesabu kesho!

**59. Jane:** Usiwe mtu wa kuahirisha mambo ambayo unaweza kuyafanya leo. Hebu tufanye hesabu kabla ya kuendelea na mambo mengine!

**60. John:** Sawa...

**61. ATMO:** *We hear him leafing through a notebook...*

**62. John:** Kwa lugha ya biashara, hii ndiyo faida tuliyopata ... jumla ya pato... ukiondoa mtaji wa kuanzisha biashara...gharamal...na

hasara... tunasalia na faida ya faranga  
93,400.

- 63. Jane:** Faida ya faranga 93,400?
- 64. John:** Tunahitaji kufungua akaunti kwenye benki ili tuweze kuhifadhi fedha zetu vizuri.
- 65. Jane:** Wazo zuri! Lakini nafikiri benki inayotoa mikopo kwa wafanyi bishara wadogo wadogo inaweza kutufaa sana sisi. Unazijua benki hizi.? Tunaweza kuulizia kesho. Lakini John wewe hujifunza wapi masuala haya ya Uchumi. Nadhani sasa ni bora tuijunge na chuo cha mafunzo ya biashara na Uchumi?.
- 66. John:** Nimefanya utafiti kidogo. Lakini wewe ni mwerevu wa kuvumbua mambo Jane.! Unapasa kusomea masuala ya biashara.
- 67. Jane:** Nitafikiria suala hilo..! Tulale sasa, tuone mambo yatakavyokwenda kesho...
- 68. John:** Tuombe tusiingiliwe na mnyama hatari tukilala...

- 69. ATMO:** *John turns out the light, pretends to be a monster and teases his sister. The cat meows even more.*
- 70. John:** (*pretending to be a monster*)  
Huuuuu... ! Huuuu! huuuuuuuu...!
- 71. Jane:** (*Unable to stop laughing*)  
Tosha ...tosha John...! tulale sasa ni usiku,  
Utamuamusha Baba amelala....!

### Outro

**NARRATOR:** Na hadi hapo msikilizaji tunafika mwisho wa makala ya leo ambapo John na Jane wanakamilisha likizo yao. Kwa kutumia ujuzi wao wa biashara, wawili hao wamefanikiwa kuwashawishi wateja kununua njugu zao na kutengeneza faida kubwa .  
Sasa wanafanya mipango ya kufungua akaunti ya benki kuweka pesa zao kabla ya kurudi shulenii. Ili kujua mengi kuhusu wanabiashara hawa, kumbuka kuungana nasi kwa kipindi kijacho cha Learning By Ear “Noa Bongo jenga maisha yako” Pia ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea mtandao wetu wa **dw-world.de/I b e**. Ukiwa na maoni pia usisite kutuandikia nasi hapa Bonn tutafurahi kuyapokea. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.

END